# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA SITA

**02 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 02 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**196. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la Ajira kwa Vijana.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**197. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga mitaro ya kuchepusha maji katika Kata za Bulyanghulu, Segese, Ngaya na Bulige.

**198. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la upungufu wa Madawati katika Shule za Msingi na Sekondari – Mwibara.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**199. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Serikali itakamilisha mwongozo wa kutoa kipaumbele cha ajira zinazotangazwa kwa wanaojitolea.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**200. MHESHIMIWA ASK. JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini ahadi ya kupeleka fedha za ujenzi wa Mito iliyopanuka katika Jimbo la Kawe itatekelezwa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**201. MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza wizi kwa baadhi ya Makatibu wa AMCOSS kwenye malipo ya Wakulima wa Korosho.

**WIZARA YA UJENZI:**

**202. MHESHIMIWA OMAR MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kuna mpango mkakati upi wa kumsimamia Mkandarasi anayejenga Barabara ya Handeni kwenda Mafuleta Km 20 kukamilisha kwa muda.

**203. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, nini mpango wa Serikali kujenga Barabara ya Manyoni East – Heka - Sanza - Chali Igongo - Bihawana - Dodoma Mjini kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MAJI:**

**204. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha vyanzo vinavyotiririsha maji Bwawa la Nyerere vinahifadhiwa na kuwa endelevu.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**205. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Wananchi wa Kata za Milambo, Kanindo na Igombemkulu - Ulyankulu watatumia Sheria Na. 7 ya TAMISEMI badala ya Sheria Na. 9 ya Wakimbizi.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**206. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa mikopo nafuu na mafunzo ya kisasa kwa Vijana wanaojihusisha na shughuli za Ufugaji na Uvuvi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**207. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya uvamizi wa Tembo katika mashamba ya Vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Swagaswaga Wilayani Chemba.

**208. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji wa Watalii kwenye maeneo ya Hifadhi.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**209. MHESHIMIWA MUNIRA MUSTAPHA KHATIB (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Sekta ya Sanaa, Michezo na Burudani kuwa chanzo cha ajira kwa Vijana.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MADINI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **02 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |